

Uhusiano kati ya Cheo Kimefutwa, Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ya 2004 na Mapambano ya Wafanyakazi

Na Laetitia Mukurasi

Nilipochapisha kwa mara ya kwanza *Cheo Kimefutwa Harakati za Mwanamke mmoja Kupigania Haki za Ajira Nchini Tanzania* mwaka 1991, nilijua nimeingia kwenye eneo lisiloeleweka. Kitabu hiki kilisimulia mateso yangu baada ya kufukuzwa ghafla kazini, ulioelezwa kwa maneno mafupi: “*Cheo chako kimefutwa mara moja*”. Kesi hiyo ilichochea moja ya mapambano makubwa ya haki za ajira Tanzania. Hadithi yangu iliigusa jamii kwa sababu haikuzungumzia tu ukosefu wa haki, bali pia udhaifu wa mfumo uliowaacha wafanyakazi wakiatarishiwa maisha yao kwa maamuzi ya kiholela. Kwa wafanyakazi wengi, kitabu hiki kiligusia uzoefu walioufahamu sana: kufukuzwa ghafla, suluhisho zisizoridhisha, kunyamazishwa kwa fikra kinzani na ubaguzi dhidi ya wanawake sehemu za kazi. *Cheo Kimefutwa* kilichangia mijadala ya kitaifa iliyochangia mageuzi ya sheria za ajira, ikiwemo Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ya mwaka 2004.

Miaka arobaini baada ya kufukuzwa kwangu, niliandika toleo la pili la *Cheo Kimefutwa* mwaka 2023. Kitabu hakiangalii yaliyopita tu bali linatazama ahadi ya Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ya mwaka 2004, mafanikio yake na mapungufu yake. Ni tafakuri ya kibinafsi na pia ya kisiasa: sheria imebadilika, lakini mapambano bado yanaendelea.

Wafanyakazi walinufaika kutokana na Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini? Mafanikio yaliyopatikana kutokana na sheria hiyo hayawezi kukanushwa: ilikuwa ni hatua kubwa katika historia ya ajira nchini. Kwa mara ya kwanza kulikuwa na mfumo wa kina ulioboresha mahusiano ya ajira baada ya miongo ya sheria zilizogawanyika. Baadhi ya manufaa yake muhimu zaidi ni:

1. **Utaratibu wa utatuzi wa migogoro** – Kuanzishwa kwa Tume ya Upatanishi na Usuluhishi (CMA) kulikusudia kuondoa ucheleweshaji kwa kutoa jukwaa rahisi kwa wafanyakazi kuwasilisha malalamiko na kupata suluhu, hivyo kuwapa tumaini kwamba haki inaweza kutolewa kwa haraka na kwa haki.
2. **Viwango vya chini vya ajira** – Sheria iliweka masharti ya wazi kuhusu saa za kazi, likizo ya mwaka, likizo ya uzazi na malipo ya kiinua mgongo. Masharti haya yalifanya haki ambazo hapo awali zilitegemea ridhaa ya mwajiri kuwa za kisheria.
3. **Utambuzi wa mgogoro wa ajira na mfanyakazi mmoja** – Sheria iliruhusu wafanyakazi binafsi, katika ngazi yoyote, kudai haki zao wakiwa na au bila msaada wa chama cha wafanyakazi.
4. **Haki ya kuunda na kujadiliana kwa pamoja** – Sheria iliimarisha vyama vya wafanyakazi kwa kuvipa hadhi ya kisheria ya kuwakilisha wafanyakazi, kujadiliana mikataba ya pamoja na hata kuchukua hatua za mgomo.
5. **Ulinzi wa kisheria wa kina kwa wanawake** – Sheria ilipiga marufuku ubaguzi, unyanyasaji wa kingono, kufukuzwa kwa uonevu na mazingira hatarishi ya kazi, huku ikihakikisha haki za wanawake za likizo ya uzazi na mshahara sawa.
6. **Mabadiliko ya uwiano wa nguvu** – Sheria iliashiria kuachana na mifumo ya kiimla ya ajira ya zamani. Iliithibitisha kwamba ajira siyo tu upendeleo unaotolewa na mwajiri bali ni uhusiano wa kimkataba unaosimamiwa na haki na wajibu kwa pande zote mbili.

Kwa wafanyakazi, mageuzi haya yalikuwa makubwa. Yalimaanisha kwamba kufukuzwa kazi kunaweza kupingwa, malalamiko yangeweza kushughulikiwa kitaasisi na waajiri wasingeweza kutenda bila mipaka kama ilivyokuwa zamani. Wafanyakazi wengi, hasa katika utumishi wa umma na makampuni binafsi makubwa, waliweza kutumia Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini kupata fidia au kurejeshwa kazini walipodhulumiwa. Mafanikio haya hayawezi kupuuzwa. Kwa namna fulani, Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ilileta uhalisia wa yale ambayo *Cheo Kimefutwa* iliyatabiri. Mapambano yangu dhidi ya kufukuzwa kwa dhuluma hayakuwa tena hadithi yangu peke yangu bali sehemu ya mfumo mpana wa kisheria uliokusudiwa kumlinda kila mfanyakazi nchini Tanzania. Hata hivyo, kama *Cheo Kimefutwa (2023)* kinavyoeleza, kuwepo kwa sheria si sawa na utekelezaji wa haki.

Pengo Kati ya Sheria na Uhalisia. Uzoefu wa wafanyakazi wengi unaonyesha pengo kati ya haki kwenye karatasi na haki katika vitendo. Wafanyakazi wanaoshinda kesi katika Kamisheni ya Usuluhishi na Uamuzi au Mahakama Kuu ya Kazi mara nyingi husubiri miaka kupata fidia. Waajiri wengine wanakaidi moja kwa moja maagizo ya kuwarejesha wafanyakazi kazini, wakichagua badala yake kulipa fidia ndogo isiyolingana na madhara yaliyosababishwa. Ushindi wa kisheria, kama *Cheo Kimefutwa* inavyoonyesha, unaweza usitafsiriwe katika haki halisi. Kizingiti kile kile cha zamani - “*kushinda kisheria lakini kushindwa kiuhalisia*” - bado kipo hadi leo.

Kutokuwa na Uhakika wa Ajira na Ajira za Muda Mfupi. Moja ya changamoto kali zaidi ni kutokuwa na uhakika wa ajira. Waajiri wanazidi kutegemea mikataba ya muda mfupi, kazi za kufanyia nje ya ofisi (outsourcing) na ajira za muda ili kuepuka majukumu ya ajira za kudumu. Wafanyakazi huwekwa kwenye kipindi cha majaribio kinachoendelea kwa muda mrefu au mikataba inayoweza kuhuishwa bila kikomo na isiyo na uthabiti. Hii si kinyume na sheria kwa kuwa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini inatambua mikataba ya muda. Lakini kwa vitendo, kipengele hiki kimeruhusu mfumo wa ajira za muda kuenea kwenye sekta mbalimbali na kudhoofisha takwa la usalama wa ajira ambayo sheria ilikusudia kuliimarisha. Wanawake na vijana ndio waathirika wakuu kwa kuwa wengi wao wako kwenye ajira zenye mishahara midogo na zisizo na uhakika. Kufukuzwa kwangu kazi kulikojengwa kwa hoja ya “cheo kimefutwa” kunalingana na mazoea ya sasa ambapo mageuzi katika taasisi au kupunguzwa wafanyakazi hutumika kama kisingizio cha kufukuza watu. Majina hubadilika, lakini uhalisia wa kutokuwa na uhakika unabaki pale pale.

Kutengwa kwa Sekta Isiyo Rasmi. Pengine udhaifu mkubwa zaidi wa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ni upeo wake mdogo. Zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania wanafanya kazi katika sekta isiyo rasmi - kama wafanyakazi wa ndani, wauza mitaani, vibarua wa kilimo na ujenzi. Kwao hawa, Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ni maandiko ya mbali yasiyo na uhusiano na maisha yao. Bila mikataba, stakabadhi za malipo au waajiri rasmi, wafanyakazi hawa hubaki wakinyonywa. Wanatengwa kwenye vyombo vya utatuzi wa migogoro kwa sababu wanakosa nyaraka za kuthibitisha uhusiano wa ajira. *Cheo Kimefutwa* ilionya kwamba sheria inayowapuuza wanyonge inaweza kuwa chombo cha kuwanyima haki. Miaka ishirini baadaye, onyo hilo bado ni sahihi. Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini imeimarisha ulinzi kwa walio ndani ya sekta rasmi lakini haijabadilisha hali ya walioko nje yake.

Ubaguzi na Unyanyasaji wa Kijinsia. Changamoto nyingine inayoendelea ni ukosefu wa usawa wa kijinsia. Wanawake bado wanakumbana na vikwazo katika ajira, kutokupandishwa vyeo na malipo duni. Tafiti zinathibitisha kwamba wanawake wanalipwa chini ya wanaume kwa kazi sawa na kwamba wamebaki wakijikita katika sekta zenye mishahara midogo zaidi. Ingawa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini inatoa likizo ya uzazi, uhalisia ni kwamba wanawake wengi wameripoti kufukuzwa, kushushwa vyeo au kuwekwa pembeni baada ya ujauzito. Unyanyasaji na ukatili wa kijinsia sehemu za kazi pia vimeenea, lakini udhaifu wa utekelezaji na tamaduni za kunyamazishwa vinawafanya wanawake wengi washindwe kudai haki. Kama nilivyodai katika kitabu changu, nia ya mwajiri kuninyamazisha ndio iliyochochea mapambano yangu. Kunyamazishwa huku bado kunaendelea hata leo. Hii inaonyesha kwamba mageuzi ya kisheria, ingawa ni muhimu, hayawezi yenyewe kuvunja mizizi ya udhalilishaji wa kijinsia.

Udhaifu wa vyama vya wafanyakazi na hofu ya visasi. Ingawa vyama vya wafanyakazi, vinatambulika kisheria, mara nyingi vinahangaika kutokana na mgawanyiko na kuingiliwa. Uanachama umebaki chini, hasa katika sekta isiyo rasmi. Wafanyakazi wanaojaribu au kuandaa wenzao kujiunga hutishiwa kufukuzwa au kuwekwa kwenye orodha ya watu wasiotakiwa. Hali hii ya hofu inadhoofisha nguvu ya maridhiano iliyokusudiwa na Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini. Bila vyama imara, wafanyakazi hubaki wakinyanyaswa na waajiri. Msisitizo wangu kwamba mshikamano ni kiini cha haki unabaki muhimu leo kama ulivyokuwa mapema miaka ya 1990.

Kuongezeka kwa Gharama na Pengo la Mishahara. Hata pale ambapo sheria inaheshimiwa, hali halisi ya kiuchumi inadhoofisha ahadi yake. Kiwango cha chini cha mishahara kinatofautiana kati ya TZS 140,000 kwa mwezi kwenye kilimo hadi TZS 592,000 maofisini wakati makadirio ya gharama za maisha ya mtu mmoja yanazidi TZS 1,200,000. Pengo hili linamaanisha kwamba kufuata sheria, hakuhakikishi maisha yenye staha. Wafanyakazi wanaweza kufurahia ulinzi wa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, lakini bila mishahara ya kutosha hubaki kwenye mtego wa umasikini. Kesi yangu ilionyesha namna uhalali bila haki unavyoshindwa kuwalinda wafanyakazi. Leo, uhalali wa mishahara midogo unarudia mgongano uleule.

Changamoto Mpya – Kazi za Kidijitali (Gig Work). Changamoto ambayo haikutarajiwa mwaka 2004 ni kuibuka kwa uchumi wa kidijitali (gig economy). Maelfu ya vijana Watanzania sasa wanafanya kazi kama madereva, wapakiaji wa mizigo au wasafirishaji wa bidhaa na wafanyakazi mtandaoni kupitia majukwaa ya kidijitali. Lakini mara nyingi hutambulishwa kama makontrakta binafsi na hivyo hukosa ulinzi wa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini. Utafiti unaonyesha kuwa wafanyakazi hawa wanakabiliwa na malipo madogo, mazingira hatarishi, kutopata likizo ya malipo na kukosa ulinzi wa kijamii. Wanaishi katika hali ya kutokuwa na uhakika wa kudumu kuhusu ajira au kipato, hali sawa na ile niliyoiandika kwenye *Cheo Kimefutwa*: bonyeza kitufe kimoja tu, ujumbe mfupi au “kufutwa akaunti” na wanaingia kwenye hali ya ufukara.

Kukabidhi kijiti. Kwa kurejea *Cheo Kimefutwa* mwaka 2023, nilionyesha kwamba mapambano yangu hayakuwa ya kibinafsi tu. Yalikuwa na bado ni mfano wa matatizo ya kimsingi yanayoendelea kuwakabili wafanyakazi wa Tanzania. Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ilikuwa hatua kubwa, lakini haijaondoa udhaifu uliotambulika kwenye simulizi yangu. Kitabu changu kinasisitiza kwamba haki lazima zisogezwe kutoka kwenye vitabu vya sheria na maamuzi ya mahakama hadi utekelezaji halisi na kutoka ahadi za kisheria hadi uhalisia wa maisha ya wafanyakazi.

Kinatoa wito kwa wafanyakazi wa leo, vyama, watunga sera na wanaharakati *kukabidhi kijiti* cha mapambano yasiyokamilika kwa ajili ya heshima kazini. Hatimaye, *Cheo Kimefutwa* ni kioo cha mapambano yasiyoisha, ni wito wa umakini na ni ushahidi kwamba mageuzi ya kisheria lazima yatafsiriwe kuwa utetezi wa haki wa kweli. Mpaka hapo mambo hayo yatakapofanywa, wafanyakazi wa Tanzania wataendelea kuishi, kama nilivyoishi mimi - kwa barua moja ya kufukuzwa au mkataba mmoja kufutwa na kuangukia kwenye ufukara

PATA NAKALA YAKO

Cheo Kimefutwa: Harakati za Mwanamke mmoja Kupigania Haki za Ajira Nchini Tanzania
(2023) kinapatikana kwenye maduka ya vitabu yafuatayo:

- **Tanzania Publishing House**, Samora Machel Avenue
- **House of Wisdom**, NHS House, Ghorofa ya Mezzanine No. 22, Samora Machel Avenue
- **Elite Bookstore**, Bagamoyo Road karibu na CRDB Mbezi Beach

letticornelius@gmail.com

+255742999944 (WhatsApp and SMS only)